



Tarehe: 19/06//2022

## TANGAZO

### UUZWAJI WA BIASHARA ZA JUMLA ZA MAZAO YA SHAMBA NA NAFAKA KATIKA MASOKO YA CHUNO NA SOKO KUU.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani anapenda kuwatangazia wafanyabaishara na wananchi wote kuwa kuanzia tarehe **20/06/2022** biashara zote za jumla za mazao ya shamba zikiwemo mbogamboga, nyanya, viazi, vitunguu, matunda, ndizi, mihogo na mazao mengine ya shamba zitashushiwa na kuuziwa katika soko la Chuno huku biashara za jumla za nafaka zitashushiwa na kuuziwa soko kuu.

Mkurugenzi pia anawakumbusha wafanyabaishara wote wanaodaiwa madeni ya kodi ya mabanda ya biashara eneo la soko kuu, soko la Kiyangu, eneo la Skoya pamoja na stendi ya zamani na Chipuputa kuhakikisha wanalipa madeni yote kabla ya tarehe **24/06/2022**, kinyume na hapo hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa banda la biashara.

Ili kuepuka usumbufu wafanyabiashara wote wanaoleta bidhaa za jumla zilizo rodheshwa hapo juu wanatakiwa kutii agizo hili ili kuijenga Manispaa yetu ya Mtwara-Mikindani.

**“Sensa kwa Maendeleo, Tujiandae Kuhesabiwa “**

Limetolewa na :-

**OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA-MIKINDANI.**



---

Kiwanja Na 168 na 171 Kitalu "K" Chikongola, Makutano ya Barabara ya Tanu na Chikongola, S.L.P 92,  
Mtwara. Simu: +255 232333102, Nukushi +255 23 2334794  
Baruapepe: [md@mtwaramikindanimc.go.tz](mailto:md@mtwaramikindanimc.go.tz) Tovuti: [www.mtwaramikindanimc.go.tz](http://www.mtwaramikindanimc.go.tz)